## AckySHINE.com

# Sheria zinazohusiana na ndoa za kulazimishwa

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Sheria ya msingi ya ndoa nchini Tanzania ni Sheria ya ndoa ya Bunge, iliyopitishwa mwaka 1971. Sheria hii inakataza ndoa za kulazimisha. Inatambua ndoa kama ni muungano kati ya mume na mke ambao kwa hiari yao wameamua kuishi kama mume na mke. Sheria hiyo inasema kwamba iwapo ndoa haikuwa ya hiari, basi hiyo siyo ndoa. Sheria pia imefafanua utoaji wa adhabu kwa watu wote wanaoshawishi au wanaolazimisha pande hizo mbili kuingia katika ndoa bila hiari yao. Kwa hiyo mwathiriwa wa ndoa ya kulazimishwa anatakiwa kutoa taarifa juu ya wale wote waliomlazimisha katika ndoa kwa polisi ambaye atawashitaki kwa kuwa hili ni kosa la jinai.